# *Uhalisiamazingaombwe* katika Fasihi ya Kiswahili: Istilahi Mpya, Mtindo Mkongwe

**F.E.M.K. Senkoro**


## Ikisiri

Makala hii inaichambua dhana ya *Uhalisiamazingaombwe* kama ambavyo imekuja kutumika hivi karibuni miongoni mwa wandishi na wahakiki wa fasihi ya Kiswahili. Pamoja na kutoa mifano ya kazi mbalimbali za fasihi ya Kiswahili ambamo mna mtindo wa Uhalisiamazingaombwe, uchambuzi katika makala hii unatumia zaidi hadithi fupi ya Said Ahmed Mohamed ya "Sadiki Ukipenda" na riwaya fupi ya E. Kezilahabi ya *Nagona* kama vielelezo vya namna *Uhalisiamazingaombwe* ulivyotumika katika kazi za fasihi ya Kiswahili. Swali ambalo makala hii inaliibua na kujaribu kulijibu ni je, ni kweli kuwa, kama anavyodai Said Ahmed Mohamed, *Uhalisiamazingaombwe* ni mtindo wa hivi karibuni tu na kwamba ndiyo kwanza dhana hii imeanza kushika kasi miongoni mwa waandishi wa fasihi ya Kiswahili, au ni istilahi mpya tu inayoelezea mtindo mkongwe?


## Utangulizi

Katika "Dibaji" ya kitabu chake cha mkusanyo wa hadithi fupi cha *Sadiki Ukipenda na Hadithi Nyingine* (Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation, 2002) Said A. Mohamed anasema yafuatayo kuhusu mtindo wa *Uhalisiamazingaombwe* alioutumia kuandikia hadithi inayobeba kichwa cha diwani yake:

> *Sadiki Ukipenda* si hadithi niliyoiandika mwanzo kamwe. Kusema kweli ni mojawapo ya zile nilizoziandika mwishomwisho labda mwaka 1987. Lakini imepata heshima katika mkusanyo huu kuja mwanzo, kwani anuani yake ni yenye mnaso wa kuweza kuifanya anuani ya mkusanyo mzima. Tena imepata nafasi ya kutumika kama anuani kwa sababu ya mtindo wake wa *Uhalisiamazingaombwe*, mtindo unaozidi kuwa maarufu katika fasihi ya Kiswahili. Na kwa hivyo hadithi hii inawakilisha kielelezo cha kubadilika kwangu (uk.vi).

Dhana ya *Uhalisiamazingaombwe* kama inavyotumiwa nyakati hizi na wandishi na wahakiki wa fasihi ya Kiswahili inaweza kutafsiriwa kwa njia mbalimbali. Katika makala hii, pamoja na kutumia mifano ya kazi mbalimbali za fasihi ya Kiswahili ambazo tunafikiri zilishatumia mtindo huu wa *Uhalisiamazingaombwe* tangu siku nyingi, tunatumia zaidi hadithi fupi ya Said Ahmed Mohamed ya "Sadiki Ukipenda" na riwaya fupi ya E. Kezilahabi ya *Nagona* – kazi ambazo ni vielelezo

vya namna *Uhalisiamazingaombwe* ulivyotumika na unavyoendelea kutumika katika kazi za fasihi ya Kiswahili. Mjadala wetu unaelekezwa katika kuyachambua madai ya Said Ahmed Mohamed katika dondoo hilo hapo juu kuhusu upya wa *Uhalisiamazingaombwe* katika kazi za fasihi ya Kiswahili.

## Muktadha wa kihistoria

Kwa vile dhana ya *Uhalisiamazingaombwe* ambayo kwa Kiingereza ni *Magic Realism* ni istilahi ambayo ilianza kutumika ughaibuni, hasa kuhusiana na utanzu wa riwaya, kabla ya kutumiwa na Said Ahmed Mohamed na waliomfuatia, tunaona ni vizuri kuiweka dhana hii katika muktadha wa kihistoria kwa kuangalia kwa muhtasari tu namna historia ya riwaya za ughaibuni ilivyopitia miongo mbalimbali hadi kufikia matumizi ya mtindo wa *Uhalisiamazingaombwe*. Tutaiangalia historia hii sambamba na muhtasari wa historia ya riwaya ya Kiswahili kwa kuichambua kama kazi za kifasihi miongoni mwa riwaya za dunia. Baada ya hapo tutazitumia kazi mbili tulizoziteua kujadili matumizi ya *Uhalisiamazingaombwe* katika fasihi ya Kiswahili kabla ya kumalizia makala kwa mjadala wa kichokozi kuhusu "upya" wa dhana hii katika fasihi hii.

Historia ya riwaya ya ughaibuni inaambatana na kukua kwa riwaya hiyo tangu riwaya za mwanzo za kiuhalisia hadi riwaya za baadaye za majaribio ya *Uhalisiamazingaombwe*. Maana ya asili ya neno la Kiingereza la riwaya, *"Novel"*, ni "kitu kipya au habari mpya." Istilahi hii ilitumika kwa jumla katika karne ya 18 kuelezea aina ya fasihi ambayo ilitokana na epiki na kazi za ulimbwende huku ikijumuisha vipengele vilivyochotwa kutoka katika aina zingine za maandishi kama vile shajara na sira zilizozingatia maisha ya mtu binafsi. Mfano mzuri ni wa riwaya za Robinson *Crusoe* (1719) na *Tom Jones* (1749). Hata hivyo, riwaya za mwanzo kabisa zilichapishwa Japani, kwa mfano ile ya Genji ya karne ya 11, na pia za Uchina za karne ya 14.

Katika kukidhi mahitaji ya kifasihi na kisanaa ya hadhira mpya ya wasomaji – hasa yale ya maisha ya mtu binafsi na hali halisi zilizozoeleka katika jamii, riwaya ilianza kushika kasi ughaibuni, sawa na ilivyokwishakutokea katika nchi za Mashariki. Waandishi wa Kispaniola kama vile Cervantes na riwaya yake ya *Don Quixote de la Mancha* (1605, 1615) waliongoza njia. Katika karne ya 19 waandishi kama vile Scott, Jane Austen, dada wawili wa Brontë, Dickens, George Eliot, Balzac, Zola, Dostoevsky, Tolstoy, Melville, na Harriet Beecher Stowe walisaidia sana kuipa nafasi riwaya ishughulikie masuala ya kimsingi ya maadili na ya ubunifu kwa wakati ule, hasa kwa vile ubepari sasa ulishajikita mizizi yake katika jamii mbalimbali, kukawa na viwanda na wafanyakazi wenye kujua kusoma na kuandika. Kuhusu kuzuka kwa riwaya, Senkoro (1982:71-72) anasema:

> Riwaya ilizuka kutokana na maendeleo na mageuzi ya kitamaduni na viwanda. Suala la ukoloni na "uvumbuzi" pia liliumba hali ambazo zilihitaji kuelezwa kwa mawanda mapana zaidi ya yale ya ngano na hadithi

> fupi. Hapohapo, kuzuka kwa miji na viwanda pamoja na maendeleo ya usomaji yalifanya riwaya nyingi ziandikwe. Uchangamano wa maisha ya jamii kisiasa, kiutamadani na kiuchumi wenyewe ulizusha haja ya kuwa na utanzu wa fasihi ulio na uchangamano kifani na kimaudhui. Kupanuka kwa usomaji, hasa wakati wa mapinduzi ya viwanda huko Uingereza kuliwafanya waandishi waandike maandiko marefu... riwaya ni utanzu ambao kuzuka kwake kulifungamana na kuzuka kwa ubepari...

Mawazo haya kuhusu kuzuka kwa riwaya yameelezwa pia na I. Watt (1976), ambaye ameonyesha kuwa, pamoja na kubakia na majukumu ya kimaadili na kiujumi, riwaya ya karne ya 20 ilipanua mawanda yake kutokana na majaribio mbalimbali yaliyofanywa na wanariwaya kama vile James Joyce, Proust, Virginia Woolf, Vladimir Nabokov, Cortazar, na Calvino. Mchango mkubwa ambao uliyapanua mawanda ya riwaya ni ule uliofanyika katika nusu ya pili ya karne ya 20 ukiongozwa na waandishi wa Marekani ya Kusini kama vile Carlos Fuentes (*The Death of Artemio Cruz*, 1962), Mario Vargas Llosa (*The Time of the Hero*, 1966), na Gabriel Garcia Marquez (*One Hundred Years of Solitude*, 1970). Mtindo wao mpya wa *Uhalisiamazingaombwe* ulivuka mipaka ya ulimwengu tuujuao kwa kupitia katika "mazingaombwe" yasiyo na wakati maalumu pamoja na uhalisi wa maisha uliochanganyikana na uajabuajabu wa mambo ambayo katika hali ya kawaida hayaaminiki kutokea.

### *Uhalisiamazingaombwe*

*Uhalisiamazingaombwe* ni mtindo au aina ya fasihi ambamo mazingaombwe/uchawi au mambo ambayo hayafanani na ya kawaida yaliyozoeleka kwa hadhira hutokea sambamba na yale ambayo ni ya kawaida. Yote haya hutokea katika mandhari au mazingira ambayo kwa kiasi kikubwa sana yana uhalisi tunaoujua. Istilahi hii imetumika kwa wingi sana katika fasihi, sanaa, na filamu.

Istilahi hii inavyotumika leo kwa hakika ni ya maelezo tu zaidi ya kuwa ya kihakiki. Matthew Strecher (1999:267) anaueleza *Uhalisiamazingaombwe* kuwa ni "yale mambo ambayo hutokea pale ambapo mandhari na matukio ya kihalisi yanavamiwa na jambo ambalo ni la ajabu mno na ni vigumu kuaminika".

Katika Kiingereza istilahi hii ilitumiwa mwanzoni na mhakiki wa sanaa wa Kijerumani, Franz Roh, alipokuwa akitoa maelezo ya picha iliyoonyesha *uhalisi uliopindwa*. Baadaye istilahi hii ilitumiwa na Arturo Uslar-Pietri kutoka Venezuela alipokuwa akihakiki kazi mbalimbali za wanafasihi wa Marekani ya Kusini waliokuwa wameutumia mtindo huu katika kazi zao. Miongoni mwa waandishi hao, kama ilivyokwisha kutajwa, alikuwemo Gabriel Garcia Marquez ambaye alikiri kabisa kuwa tatizo kubwa alilokuwa anajaribu kulitatua alipokuwa anaandika riwaya yake ndefu ya *A Hundred Years of Solitude*, ni lile la kuufuta kabisa mstari unaogawa mambo yanayoonekana kuwa ya kiuhalisi na yale yanayofikirika kuwa si ya kiuhalisi.

Hata hivyo, mhakiki kutoka Mexico, Luis Leal amesema yafuatayo kuhusu *Uhalisiamazingaombwe*:

> "Without thinking of the concept of magical realism, each writer gives expression to a reality he observes in the people. To me, magical realism is an attitude on the part of the characters in the novel toward the world, or toward nature. ..If you can explain it, then it's not magical realism.
> (Bila kufikiria dhana ya *Uhalisiamazingaombwe*, kila mwandishi anatoa maelezo ya uhalisi ambao anaung'amua kwa watu. Kwangu mimi, *Uhalisiamazingaombwe* ni mkabala kwa upande wa wahusika ndani ya riwaya walio nao kuhusu dunia... Kama unaweza kuyaeleza yanayotokea ndani ya riwaya, basi si *Uhalisiamazingaombwe*.)

Baadhi ya istilahi nyingine ambazo tunaweza kuzitumia ni zile za *fantasia* na *uchawi*. Kwa hakika, neno la Kiingereza la *magic* linakaribia zaidi maana ya uchawi badala ya neno la Kiswahili la *mazingaombwe*. Fantasia inamaanisha uundaji wa ulimwengu au dunia mpya na hata sayari mpya. Unapochunguza kwa undani maandishi kama yale ya Garcia Marquez ambaye anatumia Uhalisiamazingaombwe, utaona kuwa katika maandishi hayo hakuna dunia mpya, bali kuna mazingaombwe au uchawi ndani ya hiyo dunia.

Sambamba na fasihi nyingine za dunia, riwaya ya Kiswahili pia ilipitia hatua karibu sawa na hizo zilizotolewa muhtasari hapo juu. Tangu riwaya za mwanzo ambazo zilikuwa za kutafsiriwa, ikiwemo ile ya *Robinson Kruso*, hadi riwaya ambayo inaelezwa kuwa ndiyo riwaya ya kwanza ya Kiswahili, ya James Mbotela ya *Uhuru wa Watumwa* hadi kufikia riwaya fupi za Shaaban Robert za *Kusadikika* (1951) na *Kufikirika* (1969), na zile ndefu kiasi za *Siku ya Watenzi Wote* (1968), *Utubora Mkulima* (1968), na *Adili na Nduguze* (1972); na hatimaye za waandishi wengine kama vile Muhammed Said Abdulla, Shafi Adam Shafi, E.Mbogo, K. Mkangi, W.E. Mkufya, E. Kezilahabi na Said Ahmed Mohamed, nguvu mbalimbali za kijamii ziliainisha riwaya hizi. Kwa mfano, ilibidi Shaaban Robert atumie mficho wa kitashtiti kupitia katika kejeli na dhihaka pamoja na mambo ya uajabuajabu ili kukwepa udhibiti ambao ungeweaza kuzifanya zipigwe marufuku riwaya zake zilizoeleza mabaya ya utawala wa kikoloni.

*Uhalisiamazingaombwe* umetumika katika *Nagona* na "Sadiki Ukipenda" kwa njia zinazofanana kwa kiasi kikubwa. Zote hizi ni kazi ambazo ukiondoa maajabuajabu yanayojitokeza, unabaki na visa ambavyo ni vya kawaida tulivyovizoea.

Katika *Nagona* kuna mhusika ambaye, pamoja na kwamba hatuelezwi jina lake, anaweza kuwa yeyote kati yetu. Mhusika huyu ambaye ana "Umimi" wa Kimungu, yuko safarini tangu mwanzo wa hadithi hadi mwisho. Taswira hii ya safari ni ya kawaida, kwani katika dunia tuliyoizoea watu husafiri kila uchao. Hata hivyo, katika safari hii mnachomekwa matukio na wahusika ambao hawakuzoeleka katika hali ya kawaida kwani wanazuka ghaflaghafla tu. Mathalani, mhusika huyu anayesafiri hajui

ilikuwaje akafika hapo alipofika, na wala hana uhakika na hapo alipo. Ndiyo sababu riwaya hii fupi inaanza na neno "Yaelekea". Mhusika huyo ghafla anakutana na babu yake alkiyekufa zamani, babu ambaye katika mazingira ya hadithi, ana sifa za uhalisi zaidi ya wahusika wengine. Ni babu ndiye anayeandamana na mhusika huyu katika safari ya kuusaka "ukweli" ambao umo ndani ya huyo Nagona anayetarajiwa na watu wote. Ni katika safari hii ndimo ambamo mhusika huyu anakutana na wahusika wengine, wakiwemo *Id, Ego* na *Superego* – wahusika ambao majina yao yanalandana na dhana za kinafsiya au kisaikolojia zinazoaminika kuwa kwa kusaidiana ndizo zinazomkamilisha mtu.

Katika riwaya hii fupi, mwandishi ametumia ishara na taswira nyingi sana sambamba na sitiari kuu ya safari ambayo ndiyo mwimo wa hadithi. Kati ya hizo zikò za msitu mweusi na paka mweusi ambaye pamoja na mambo mengine anawakilisha mashaka, wasiwasi na mambo yasiyojulikana katika maisha, paa ambaye inaelekea ametakiwa na mwandishi awakilishe uzuri wa maisha ambao ni wa kupita tu, jogoo mwenye kuashiria kujirudiarudia kwa hali mbalimbali za maisha kiasi cha kuchusha; barabara ambayo inawakilisha urefu wa safari ya maisha isiyo na mwisho, tena yenye kupindapinda, ukichaa ambao unaweza kuwa mwendelezo tu wa namna Kezilahabi anavyoyaona maisha hata katika riwaya yake nyingine ya *Dunia Uwanja wa Fujo*; **Mimba ya Uwezo wa Roho Mtakatifu** ambayo kwa hakika inaigiza tu ile ya kwenye misahafu, ya Bikira Maria aliyemzaa Yesu Kristo au Nabii Isa – mimba ambayo imetakiwa ilete matumaini kuhusu maisha ijapokuwa pia inaashiria kuwa maisha mapya na mazuri zaidi huja baada ya kupita kwa yale ya zamani na watu au vizazi vyake; Hukumu ya Mwisho na mhusika Jitu – ishara za maana na hatima ya maisha - kifo. Humu ndimo ambamo yaelekea Kezilahabi anataka kudhihirisha kuwa maisha hayana maana kwani mtu huzaliwa ili afe.

Ni katika ishara na taswira zote hizo ndimo ambamo jawabu la fumbo la safari ya mhusika mkuu limejificha. Jawabu hili ambalo limewakutanisha Nabii, Mtume na Mwindaji linaelekeza kwenye umuhimu wa watu kutupilia mbali itikadi na imani zao na kuungana. Muungano huu wa dini umelenga kwenye kupinga mambo yanayotokea leo hii ambapo dini zimekuwa chanzo cha chuki na vita miongoni mwa jamii na mataifa mengi duniani.

Hatimaye, mwishoni mwa riwaya hii fupi kuna mashindano ya ngoma ambayo yanachezwa na watu wa itikadi mbalimbali. Mashindano haya yanafanyika katika mviringo, na kila kundi na itikadi yake linapoingia katika mviringo linaingia kwa fujo za aina yake. Humu ndimo ambamo tunakutana na wahusika-tajwa kadhaa, wakiwemo Aristotle, Darwin, Freud, Hegel, Marx, Nietzsche, Plato, Socrates na wengineo ambao katika mashindano haya wanawakilisha mitazamo na itikadi tofautitofauti. Mashindano haya yanaendelea hadi "mwanamke" aliye katikati ya mviringo anapojifungua mtoto, ndiye huyo Nagona ambaye amekuwa akisubiriwa. Mtoto huyu anayezaliwa katikati ya vurugu za mashindano ya ngoma za kiitikadi tunaweza kumchukulia kuwa ni kiwakilisho cha mfumo mpya wa jamii utakaokuja

baada ya vurugu za mifumo na itikadi ambazo dunia inazipitia sasa hivi. Ni dhahiri kuwa mtoto huyu hana budi kuzaliwa kwa kupitia katika vurugu, na vurugu hizi huweza kuwakilisha zile za kiitikadi kwani humu tunakutana na majina ya waasisi wa nadharia na itikadi mbalimbali ambao wako katika duara – wakiwemo Plato, Socrates, Aristotle, Hegel, Darwin, Marx, Freud, na Nietzsche.Mwandishi anawaita hawa kuwa ni "kikundi kidogo tu cha waliokuwa wabishi katika usakaji wa njia". Ni katika sehemu hii ambako mwandishi anatuletea uhalisi wa aina fulani anapoongelea "vita mbalimbali ambazo zinashuhudiwa duniani leo". Ni kama vile mwandishi anarudia msemo kuwa amani haipatikani hadi kwa ncha ya upanga.

Kama uchambuzi unavyoonyesha, pamoja na kwamba wahusika, matukio na mandhari ya kwenye *Nagona* huweza kuonekana kuwa ni vitu vya ajabuajabu, ndani ya uajabu huo mmejificha taswira, ishara na tamathali – hasa sitiari; maana ambazo zinahusiana na uhalisi wa maisha tunayoyaishi leo. Hiki ndicho kiini cha *Uhalisiamazingaombwe* ambacho tutakichambua kwa undani zaidi baada ya kuitalii hadithi fupi ya "Sadiki Ukipenda" yenye kufuata mtindo huohuo.

Kwa kifupi, hadithi ya "Sadiki Ukipenda" inasimulia kisa cha mhusika aitwaye Mussa ambaye ni rafiki mkubwa wa mhusika mwingine aitwaye Mzee Siwa. Kisa chenyewe kinamhusu babake Mussa ambaye ni *mchawi* anayeamua kumtoa Mussa kikoa. Mzee Siwa anamwambia Mussa:

> "Babako ni mchawi. Na sasa anadaiwa mwana. Na ye' kawaambia wachawi wenzake yu tayari kumtoa yeyote kati ya ndugu zako, ila si wewe. Lakini wenzake wamekataa. Wanataka sharti wewe, maana wewe ni msomi, na wasomi wana hatari! Kila siku wanatafuna na kuuma!" (uk.5)

Hadithi nzima imejengwa katika misingi ya mgogoro baina ya uchawi wa babake Mussa ulioko katika kumtoa kikoa mwanawe, na kago la kujikinga na uchawi huo linalotolewa na Mzee Siwa kwa Mussa.

Babake Mussa anajaribu kumtoa kikoa kijana wake, na Mzee Siwa naye anazuia jambo hili kwa kutumia mbinu za "kiuchawi" ambazo, hata hivyo, tangu mwanzo wa hadithi mwandishi anafanya kila juhudi kwa kupitia kwa mhusika Mzee Siwa tuziamini kuwa si mbinu za kiuchawi kwani Mzee Siwa si mchawi. Ili kutuhakikishia hili, kurasa tano za mwanzo zimetumika kumjenga Mzee Siwa kwa namna ambayo inatuwia vigumu kutomwamini. Twaelezwa kuwa Mzee Siwa ni mkweli. Tunatakiwa tuikubali sifa hii ya kuwa mkweli ili tumwamini Mzee Siwa kwa lolote atakalolisema. Mwandishi, kwa kupitia katika mdomo wa Mussa anasema:

> Kwake (Mzee Siwa) neno ni deni kubwa kuliko deni la fedha. Pili, ushujaa wake. Penye haki husimama kidete bila ya kutetereka wala kuwa na hofu ya mtu yeyote, mkuba au mdogo. Tatu, imani yake, hasa kwangu... Nne, uhodari na ukakamavu wake...Miongoni mwa yote yale

> nilihusudu kumsikia akisema. Ulimi wake daima ni nasaha. Kichwa chake ni maarifa. Shauri lake ni busara... Kwa kuwa kila binadamu asingalikosa ila, ila ya Mzee Siwa, kama ni ila, alijitenga makusudi na wazee wengine wa kijijini na hakuficha kuwaambia... Na kwa sababu mara zote amewapa kweli chungu wenzake basi wamefarakana naye na kumpagaza jina la *Mjuaji*! Na wengine *Mchawi*!
>
> Lakini si mimi. Mimi namjua kuwa ni mzee anayethamini utu. Kwa hivyo, asingaliweza kuwa mchawi. Na baada ya kutokea kadhia hii ninayioieleza, ndiyo kabisa nimesadiki kuwa yeye si mchawi, na kwa kweli siku zote hizi yeye amekuwa dhidi ya uchawi.

Maelezo haya na mengine yanayofuatia haya ambayo yanamweleza Mzee Siwa kuwa ni mcha Mungu, mkakamavu mwenye afya njema, na ni mtu wa kusema kweli daima, ni juhudi za makusudi kabisa za mwandishi kutufanya sisi wasomaji tumwamini Mzee Siwa kuwa ni mtu wa kawaida ambaye hata kama atafanya mambo ambayo yanaonekana kama ya kiuchawi, lakini kwa hakika yeye si mchawi.

Si katika wahusika tu, bali pia mwandishi ametupa mazingira ya kawaida ambayo hayatupi hisia ya kiuchawi, anaposema, kwa mfano:

> Adhuhuri. Jua *linaatilisha* kila kitu kilichothubutu kupita kwenye uwazi wa dunia. Mbingu zimetakatika samawati, baada ya mawingu kukimbia ukali wa jua. Ila, muda hata muda, kipepo *mwanana* kilijitahidi kuzimua vuke la joto lililong'ang'ania angani. Ng'ombe walikuwa wamejilalia malishoni kwa uzito wa machofu, wakichakua mabaki ya matafuno vinywani mwao. Muda hata muda zilisikika 'baa' zao zikikata hewa. Kunguru tu ndio waliokuwa wameshughulika kwenye wakati huu wa dhiki. Kunguru hachoki mpaka jua litue. (uk. 2)

Mandhari kama haya yanaweza kuwa katika kijiji chochote ambako jua huwaka, upepo huvuma, joto huzizima, ng'ombe hujipumzikia na kucheua baada ya malisho na kunguru huruka huku na kule angani. Ni mandhari ambayo, mbali na kupambwa na mwandihi katika maelezo yake, ni ya kawaida tu yasiyo na uajabu wowote ule. Na ni katika mazingira haya ndimo mambo ya mzazi kumtoa mwanawe kikoa na mwana mtu kupewa kago la kujikinga.

Ni katika maelezo hayo kuhusu mhusika Mzee Siwa na pia mandhari ambamo hadithi hii inatokea, ndimo tunamoona juhudi za mwandishi Said Ahmed Mohamed, sawa na zile alizozikiri Gabriel Garcia Marquez wakati wa kuandika *A Hundred Years of Solitude*, za kuuondoa mpaka uliopo baina ya *uhalisi* na *uchawi*. Mzee Siwa anawekwa sambamba na babake Mussa na wenziwe, na mazingira ya kawaida yanawekwa sambamba na yale ya kiuchawi ya, mathalani, uwezekano kwa mtu kupita ukutani na kuingia chumbani kimaajabu.

Hata kago analoliandaa Mzee Siwa, kwa kiasi kikubwa linatokana na mambo halisi kwani twaelezwa kuwa ni dawa ya mizizi fulani iliyochemshwa akapewa Mussa anywe. Na hata ile ya kufukiwa kwenye kizingiti cha chumba chake Mussa, au hirizi ya kufunga mkono wa kulia wa Mussa, vyote ni vitu vinavyoonekana, vinavyogusika, vinavyonusika.

Baada ya yote hayo, ndipo sasa mwandishi anapotuingiza katika ulimwengu wa *uchawi* wa kupasuka kwa ukuta na babake Mussa kuingia kupitia katika ufa huo uliojitokeza hadi chumbani kwa Mussa:

> ...Mara nikaona ukuta wangu wa chumba mkono wa kulia ukipasuka! Mbio, mbio, mbio nilitoka nje, nikakimbilia chini ya mbuyu. *Kazi ya kwanza niliyoagizwa na Mzee Siwa imekwishai.* Na 'mi nikajihisi kama maiti niliyefufuka (uk. 6)

Pamoja na juhudi zote za kumtoa mwanawe kikoa, kago iliyotengenezwa na Mzee Siwa inakuwa kinga kubwa hadi inawahadaa wachawi ambao wanatoa chege la mgomba na kulibeba wakidhani wamebeba mwili wa Mussa hadi huko kwenye jumuia ya wachawi. Hapa ndipo mwandishi anapotupa mazingira ambayo ni tafauti kabisa na yale aliyoyaeleza mwanzo:

> ...Basi nikamwandama baba'angu na lile zuzu lake. Mimi niliweza kuwaona, lakini wao hawakuweza kuniona...Walikwenda kitambo kirefu. Hatimaye wakafika pahala penye uwanda ambapo watu wengi walkikuwa wamekusanyika. Ilikuwa jumuia ya wachawi. Wote walikuwa uchi kama walivyozaliwa. Hawana haya. Nilimeza fundo moto na chungu la mate. Wale wachawi walipomwona baba'angu anaingilizana na ng'ombe au zuzu lake, walipayukwa kwa furaha na shangwe, na hapohapo ugoma ukadundwa...

Katika cherekochereko na ngoma za kichawi zilizoambatana na nyimbo za kutoa kikoa ndimo ambamo tunamgundua mhusika mwingine mchawi, Sheha wa kijiji, mzee Mfaki Kombo ambaye anatoa hotuba kwa wachawi wenziwe kwa sauti iliyopasua ukimya wa usiku wa manane. Kinyume na maisha ya kawaida ambayo yanamchukulia Sheha kama kiongozi mwadilifu, twaelezwa kuwa mzee Mfaki Kombo ni "kinying'inya cha marehemu Bikirembwe, malkia wa uchawi"(uk.7). Hiki ni kinyume cha mambo ambacho kinauweka uhalisi wa maisha adilifu ya sheha sambamba na maisha potovu ya *uchawi* wa sheha huyohuyo. Mwandishi hasiti kulisisitiza hili anaposema:

> Hatimaye sheha, sheha wa kijiji chetu na uchawini, alisitisha ugoma na hujuma..."Basi tena, kesha 'uyo. Kware, mrejeshe mwanao. Kesho kutwa tutakuja mchukua kwa shangwe kubwa zaidi, keshokuwa tutapokuja kukuekea chege uzike na sisi utupe mtoto tumle.(uk. 7)

Namna hadithi inavyokwisha inatuachia maswali mengi ambayo yanahitaji majibu. Ni Mussa ambaye analipa kisasi kwa kumpiga babake pigo ambalo hatimaye

linamuua. Na katikakati ya haya, nafsi ya Mussa inauliza maswali mengi: *Huendaje kufikia hivi dunia, mtu na mwanawe kuhujumiana? Ama kweli imani imekwisha. Hii ni **aheri dunia!***

Meli ambamo Mussa yumo akielekea kwenye safari ya kuuona "ulimwengu mwingine" ni ishara ya mambo na maisha mapya. Na Mussa anasema kuwa angependa kurudi pale atakapokuwa "mtu kamili " aliye huru yeye na roho yake. Twaelezwa kuwa katika meli hiyo, Mussa hayuko peke yake kwani mna vijana wengine wengi ambao hata hivyo hawajui wnaelekea wapi lakini wanajua watokako.

Hadithi ya "Sadiki ukipenda", sawa na riwaya ya *Nagona* ina sitiari iliyojazana taswira na ishara nyingi ambazo kwa juujuu huonekana kama ni uchawi. Kama tulivyosema, istilahi ya *mazingaombwe* inaelekea kusadifu zaidi ya uchawi, kwani mazingaombwe ni kiini macho tu ambacho hufanywa haraka mno kiasi kwamba huwahadaa watazamaji kuwa yatokeayo ni ya kweli. Kama kiinimacho hiki kingefanywa kwa mwendo wa polepole, watazamaji wangeweza sana kuuona uhalisi na ukawaida wake. Kuipasua sitiari hiyo vipandevipande ili kung'amua maana za taswira na ishara mbalimbali zilizomo humo ndio huo mwendo wa polepole. Inatubidi kujiuliza kwanza Mzee Siwa anawakilisha watu wa namna gani katika jamii zetu, na kinyume chake, babake Mussa, mzee Kware na *wachawi* wenziwe, akiwemo sheha wa kijiji, wanawakilisha watu wa namna gani katika jamii. Ikiwa Mzee Siwa anawakilisha watu adilifu ambao wanaitakia mema jamii, basi kago analolitengeneza linaweza kuwakilisha itikadi chanya na sahihi ambayo hatimaye itaikomboa jamii kutoka katika itikadi hasi ya *uchawi* wa kuwatoa kikoa vijana ambao ni tegemeo la jamii. Huenda tendo la kuwatoa kikoa vijana linawakilisha hali za maisha ambazo leo hii zinawakatisha tamaa vijana wanaojikuta wakilazimika kuihama nchi kwa kuzamia katika meli za kuwapeleka nje.

Kwa jumla, ishara na taswira mbalimbali za "Sadiki Ukipenda" zinaelekea kutoa taswira ya jamii ambayo imekosa mwelekeo, kwani wale ambao wanatarajiwa kuiongoza ndio hao hao wanaoiangamiza. Vitendo vya hao wanaotarajiwa kuiongoza jamii vizuri ni vile vya kifisadi na vya kuwakatisha tamaa vijana kama Mussa na hata kutaka kuwamaliza kabisa kwani ni "wasomi" ambao, kwa mawazo ya *wachawi* hao, hawana faida yoyote kwa jamii zaidi ya kuwa na "hatari" ya kila siku kutafuna na kuuma. Kutafuna na kuuma kumetakiwa kuwakilisha mawazo mapya ambayo vijana wanajaribu kuyatoa kuwa mchango wa kimaendeleo kwa jamii zao.

Tunaweza kusema kuwa "Sadiki Ukipenda" inaendeleza ile dhamira kongwe ya mvutano wa kirika, mvutano wa vizazi, ambao umeshughulikiwa na baadhi kubwa ya kazi za fasihi ya Kiswahili, zikiwemo zile za *Wakati Ukuta* (E.Hussein), *Lina Ubani* (P. Muhando), *Rosa Mistika* na *Kaptula la Marx* (E.Kezilahabi) na hata *Shida* (Ndyanao Balisidya) na *Hatia* (P. Muhando), miongoni mwa nyingi nyinginezo. Tofauti tu hapa ni kuwa wakati kazi hizi zinaonyesha mvutano huo wa pande mbili mahsusi, katika "Sadiki Ukipenda" kuna mchango wa kizazi cha zamani, mchango

muhimu wa Mzee Siwa, ambao unakiongoza kizazi kipya. Hata hivyo, mchango huu una mipaka yake, kwani unafaulu tu kuzuia mabaya ambayo kizazi cha zamani kinayanuia kwa kizazi kipya, unashindwa kuwazuia vijana kukimbia na kukimbilia nchi za nje.

Lakini pia tunaweza kulitafsiri tendo la vijana kukimbilia nchi za nje kuwa si la mwili unaoonekana na unaoshikika kuhama kutoka nchi moja kwenda nchi nyingine. Inawezekana kabisa kuwa "kuihama nchi" ni tendo la vijana kulazimika kujiingiza katika utumiaji wa madawa ya kulevya kama vile bangi au kokeni – tendo ambalo linawafanya "wahame' kutoka katika shida, taabu na madhila ya umasikini unaoletwa na *masheha wachawi* wasiowajali. Matumizi ya madawa ya kulevya yanawafanya wapate ahueni ya kusihi kwenye ulimwengu wa ndoto ambao hata hivyo huwarejesha mara nguvu za madawa hayo zinapoisha. Lakini pia, inawezekana kuwa *ukimbizi* huu ni ule wa kiitikadi; ni ule wa kuzikumbatia itikadi mbalimbali zisizo na kichwa wala miguu ambazo zinaletwa na dude liitwalo utandawazi. Dude hili linawafanya vijana hawa wasijue kwa nini wameziasi jadi zao zinazowakilishwa na Mzee Siwa, na sasa wameuparamia ulimwengu ambao hata hawaujui. Ndio maana mwishoni tunaelezwa kuhusu vijana ambao "hawajuti kwa nini wameondoka kwao, ingawa hawana uhakika na wanakokwenda".

## Mjadala wa Kuchokoza

Pamoja na kwamba katika kazi hizo za fasihi tulizozipitia harkaharaka, na pia katika kazi nyinginezo za zama hizi, kama vile za *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Vipuli vya Figo* (E.Mbogo) *Walenisi* (K. Mkangi) *Ziraili na Zinani* (W.E. Mkufya), S.A. Mohamed, S. A. (*Pungwa, Kivuli Kinaishi, Amezidi na Babu Alipofufuka*, (S.A. Mohamed), mtindo huu wa *Uhalisiamazingaombwe* umetumika, tuonavyo sisi, haimaanishi kuwa ni mtindo mpya. Kazi kama vile za Shaaban Robert za *Kusadikika, Kufikirika* na *Adili na Nduguze* ni mifano mizuri sana ya zile ambazo ni za zamani na zilizotumia mtindo huu wa *Uhalisiamazingaombwe*. Katika *Adili na Nduguze*, kwa mfano, ulimwengu wa kawaida tunaoujua unaingiliana na ule wa majini bila tatizo lolote. Adili anao uwezo wa kuzama hadi huko wanakoishi majini, katika kina cha bahari, na kuongea nao, na majini yanamtembelea na kumpa adhabu kali sana anapowahurumia wale manyani ambao ni ndugu zake waliogeuzwa tu kuwa nyani. Tendo la ndugu hawa kugeuzwa kuwa nyani ni tendo la "kiuchawi" ambalo tunapolichukulia kijuujuu tunaona kuwa haliwezekani kutokea katika maisha halisi tuliyoyazoea.

Uhalisiamazingaombwe ni mtindo wa kifasihi unaokutanisha uhalisi na mambo ambayo kwa kawaida si ya kiuhalisi. Mambo hayo ni kama sitiari ambayo inasubiri kupasuliwa ili tuzikute humo taswira na ishara zinazowakilisha uhalisi. Kwa maana hiyo basi, *Uhalisiamazingaombwe* ni makutano ya uhalisi wa kawaida na uhalisi uliojificha katika sitiari. Kwa mfano, katika sitiari ya unyani mna uhayawani ambao unawakilisha ubepari uliokuwa umeshika mizizi hata wakati wa Shaaban Robert. Ubepari huu ulionyesha na bado unaendelea kuonyesha unyama wake; ndio sababu

ndugu zake Adili wako tayari kumtumbukiza ndugu yao wa damu baharini afe na wao wamrithi mpenzi wake pamoja na mali zake zote. Ni hadi pale wanapopitia mateso na machungu ya kuchararazwa viboko kila usiku wa manane, na ni mpaka wanapokiri makosa yao kwa kuficha nyuso zao kwa aibu ndipo wanaporudia ubinadamu wao. Sasa wanavuliwa uhayawani na kuvalishwa utu wenye urazini.

Kwa juujuu hayo yote yanaweza kuonekana kama mazingaombwe kwani si kweli kuwa mtu anaweza kugeuka kuwa nyani na baadaye kugeuka tena kuwa mtu. Hili linawezekana tu kutokana na *uhuru wa kisanaa* ambao umebebwa katika dhana hii ya *Uhalisiamazingaombwe*. Hili linawezekana tu katika ishara na taswira zilizojificha ndani ya sitiari kuu, sitiari ya safari ambayo Adili na nduguze wanaifanya, sawa na vile ambavyo maluweluwe mengi yenye ukungu yaliyojificha katika sitiari ya safari kwenye *Nagona* yanageuka kuwa mambo ya kawaida tu tunapoipasua sitiari hiyo na kuanza kuzifasili taswira na ishara lukuki tunazozikuta ndani ya sitiari hiyo – kazi ambayo si rahisi sana bila kujua nyanja mbalimbali za maisha ya humuhumu duniani, zikiwemo za falsafa, dini, siasa, uchumi, na hata baadhi ya nadharia za fasihi.

## Hitimisho

Makala hii imejaribu kueleza kwa kifupi maana ya istilahi ya *Uhalisiamazingaombwe*, ikatoa vielelezo vya matumizi ya mtindo huu hasa katika riwaya ya *Nagona* na hadithi fupi ya "Sadiki Ukipenda". Imeonyeshwa kuwa, kwa jumla, kazi za fasihi ya Kiswahili za nyakati hizi, ambazo zinatumia mtindo wa *Uhalisiamazingaombwe* zinafufua tu mtindo ambao ulishazoweleka katika baadhi ya kazi za fasihi za zamani, na ambao umezoweleka hadi leo katika fasihi simulizi, hasa kwenye ngano, visasili, visakale na visajanja. Wakati ambapo kazi za nyakati hizi za Said Ahmed Mohamed, kama ile ya *Babu Alipofufuka* na za waandishi kama vile Kezilahabi na wengine zinapotumia mtindo huu inawezekana zikaonekana kuwa zina upya fulani, makala imeonyesha kuwa *Uhalisiamazingaombwe* ni istilahi mpya tu ambayo imetumika kuelezea mtindo mkongwe sana; ni babu wa mitindo ambaye sasa waandishi hawa "wanamfufua" kwa kumpa damu changa katika fasihi andishi. Lakini pia inabaki kwa wasomaji na wahakiki wengine kuamua iwapo ni sahihi kuuita *Uhalisiamazingaombwe* kuwa ni mtindo. Je, inawezekana kuwa *Uhalisiamazingaombwe* si mtindo, mkondo, wala tapo, ila ni kipengele tu cha kuunganisha fani na maudhui ya maisha halisi na yale ambayo kijuujuu yanabeba umazingaombwe?

## Tanbihi

Kwa maelezo zaidi kuhusu dhana au mtindo huu, soma Elga Perez-Laborde:"Marcela Donoso", *Jornal do Brasilia*, (1999); Elga Perez-Laborde:"Prologo",*Iconografia de Mitos y Leyendas, Marcela Donoso*, ISBN 956-291-592-1; Franz Roh: Nach-Expressionismus. Magischer Realismus. Probleme der neuesten europäischen Malerei. Klinkhardt & Biermann, Leipzig, 1925; García, Mario (2000). Luis Leal: An Auto/biography. University of Texas Press. uk. 91. Ambacho pia hupatikana katika mtandao wa http://books.google.com/books?id=9FX7JaStSxUC; na vilevile katika

mtandao kuna maelezo marefu yanayopatikana katika http://www.magicasruinas.com.ar/tapas/pichist634.htm; Matthew C. Strecher, Magical Realism and the Search for Identity in the Fiction of Murakami Haruki, *Journal of Japanese Studies*, Volume 25, Number 2 (Summer 1999) kur.. 263-298; Wendy Faris, "Scheherezade's Children: Magical Realism and Postmodern Fiction," katika Zamora na Faris, wah., *Magical Realism*, uk. 163.; Wolfe, Gene; Baber, Brendan. "Gene Wolfe Interview" katika Wright, Peter. *Shadows of the New Sun: Wolfe on Writing/Writers on Wolfe*; http://books.google.com/books?id=MkPfjCVo3g4C&pg=PA132.

## Marejeo


Hussein, E. (1969), *Kinjeketile*, Oxford University Press, Nairobi.

Hussein, E. (1971), *Mashetani*, Oxford University Press, Nairobi.

Hussein, E. (1976), *Jogoo Kijijini na Ngao za Jadi*, Oxford University Press.

Kezilahabi, E. (1974), *Kichwamaji*, East African Publishing House, Dar-es-Salaam.

Kezilahabi, E. (1975), *Dunia Uwanja wa Fujo*, East African Literature Bureau, Dar-es-Salaam.

Kezilahabi, E. (1990), *Nagona*, Dar-es-Salaam University Press, Dar-es-Salaam.

Liwenga, G. (1981), *Nyota ya Huzuni*, Tanzania Publishing House, Dar-es-Salaam.

Marquez, G.G. (1970), *One Hundred Years of Solitude*, New York: Penguin.

Mbogo, E. (1988), *Ngoma ya Ng'wanamalundi*, Education Services Centre Ltd, Dar-es-Salaam.

Mbogo, E. (1996), *Vipuli vya Figo*, East African Educational Publishers, Nairobi.

Mkangi, K. (1995), *Walenisi*, East African Educational Publishers, Nairobi.

Mkufya, W.E. (1999). *Ziraili na Zirani*, Hekima Publishers, Dar-es-salaam.

Mohamed, S. A. (1988), *Pungwa*, Longman Kenya, Nairobi.

Mohamed, S. A. (1990), *Kivuli Kinaishi*, Oxford University Press, Nairobi.

Mohamed, S. A. (1996), *Amezidi*, Oxford University Press, East African Educational Publishers, Nairobi.

Mohamed, S. A. (2001), *Babu Alipofufuka*, Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Muhando, P. (1975) *Hatia*. Nairobi: EALB.

Muhando, P. (1978) *Lina Ubani*, Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Robert, Shaaban (1951& 1991), *Kusadikika*, Nairobi: Nelson & Dar es Salaam: Mkuki na Nyota

Robert, Shaaban (1969 & 2003). *Kufikirika*, Nairobi/Dar es Salaam: Oxford & Dar es Salaam: Mkuki na Nyota

Robert, Shaaban (1972), *Adili na Nduguze*, Nairobi: Nelson.

Strecher, Mathew (1999), "Magical Realism and the Search for Identity in the Fiction of Murakami Haruki", *Journal of Japanese Studies*, Juzuu 25/2

Watt, I. (1976), *The Rise of the Novel*, Penguin, London.